**Imempasa Kupitia Mateso Mengi**
**Matthayo 16:21**
Na Phillip G. Kayser katika Kanisa la Dominion Covenant Church, Omaha NE tarehe 22-3-2015

Matt. 16:21 Toka wakati huo Yesu akaanza kuwaonyesha wanafunzi wake ya kwamba imempasa kwenda Yerusalemu, na kupitia mateso mengi katika mikono ya wazee na makuhani wakuu, na waandishi, na kuuwawa, na siku ya tatu kufufuka.

## Utangulizi

Mwaka 2011 niliwapa nadharia mpya ya kusulibiwa kwa Bwana wetu katika siku ya Alhamisi (ambayo mimi naamini ndiyo siku aliyosulibiwa). Ni moja kati ya nadharia tatu za wainjilisti ambazo zinaelezea siku kumi za mwisho za Kristo zilivyokuwa kabla ya kifo chake. Na inawezekana ulikuwa hufahamu jambo hili, lakini kwa wanateolojia, siku kumi za mwisho za maisha ya Kristo ni moja kati ya wendo (chronologies) ngumu kuzielewa na kuzieleza kwa usahihi na ufasaha. Sasa, binafsi napenda sana aina hii ya changamoto. Lakini kwa kawaida ninasita kuwahusisha katika kazi ya kutafiti kwa utondoti inayopelekea katika kutatua mafumbo kama haya. Lakini mwaka 2011 nilitoka nje ya kawaida yangu, na safari hii nitafanya hivyo tena.

Hivyo badala ya kuanza mfululizo wa mafundisho yangu kuhusu kitabu cha Ufunuo wiki hii na kusitisha mfululizo huo kwa wiki nne mara tu baada ya kuuanza, nilifikiri nianzishe mafundisho ya Wiki ya Mateso ya Kristo Jumapili hii, halafu tuichambue hulka ya ushindi ya Jumapili ya Matawi wiki ijayo, na mwisho tutazame jinsi ufufuo wa Yesu ulivyokuwa mwanzo wa kufanya kila kitu kuwa upya. Halafu ningeondoka kwa ajili ya kufanya kazi ya uandishi ya wiki mbili kama ilivyo kawaida yangu kila mwaka. Hivyo niliona ni jambo la maana kuanza mfululizo wa masomo ya Ufunuo baada ya hayo yote, hivyo kwa wale ambao wamesikitishwa na ratiba hii mpya, kuna sababu nzuri tu ya kuahirisha mfululizo ule wa Ufunuo.

Sasa, msomaji wangu utalazimika kufikiri kwa makini sana katika mafundisho ya asubuhi ya leo. Lakini nimejaribu kuyarahisisha. Nimenakili jedwali nililolitengeneza miaka mitano liliyopita ambalo linaonyesha / linarekodi alama sahihi na zisizo sahihi kwa kila hoja ya nadharia zote tatu ili kuona ni ipi inapata alama zote kwa usahihi kuhusiana na siku sahihi aliyosulibiwa Bwana wetu. Na ni matumaini yangu kwamba utaondoka hapa leo ukiwa na shukrani yingi zaidi juu ya kutokuwa na makosa kwa Maandiko, na namna nzuri kweli kweli ambayo Mungu ameyasuka pamoja matukio lukuki ya Wiki ya Mateso.

Aya tuliyoisoma sasa hivi inasema kwamba ***imempasa*** Yesu kwenda Yerusalemu na kupitia mateso mengi. Leo tutatazama baadhi ya mateso hayo mengi ambayo yamewakanganya wanazuoni. Nami nitaanza na dhana kwamba kuna mpangilio wa matukio yote ya siku zlilizofuata uliofanywa na kuhitimishwa na Mungu mwenyewe unaotokana na neno "*imempasa*". Kama kipengele kimoja tu kitakosekana au kukosewa, basi mpangilio wa matukio yote uliofanywa na Mungu kuhusiana na wiki ile hautaeleweka. Katika Marko 14:2 tunasoma kwamba Mafarisayo hawakutaka kumwua Yesu mpaka *baada* ya Karamu na mpaka *baada* ya makundi ya watu wote kuondoka. Na sababu inayotolewa ni kwamba hawakutaka kusababisha ghasia. Lakini ilimpasa Yesu kupitia kila siku ya mateso kwa sababu ilikwishatabiriwa miaka 1500 kabla. Luka anaandika kwamba *alienda kama ilivyopangwa*. Aya ya 27 ya sura hiyo hiyo inasema kwamba kuna *saa* ya kutukuzwa Kwake na Yohana 13:1 inazungumzia juu ya *saa* atakayoondoka duniani. Matukio yote kuhusiana na ile wiki *yalipangiwa mpaka saa ya kutokea kwake*. Na kuhusiana na matukio angalau matatu ya wiki hiyo,

© Copyright 2015 by Phillip G. Kayser. Permission is granted to individuals to download, print, or distribute this sermon on paper or electronically, provided that each reprint bears this copyright notice, current address, and telephone number, and provided that all such reproductions are distributed without charge. They may not be sold or issued in book form, CD-ROM form, or microfiche without prior permission. All rights reserved.
Phillip G. Kayser • Dominion Covenant Church • 307.N 41st Ave. Omaha, NE 68131 • 402.934.3300

matukio yake yalipangiwa mpaka *dakika* ya kutokea kwake. Huwa nashikwa na tetemeko hadi moyoni mwangu pale ninapotafakari juu ya mpangilio wa matukio ya Wiki ya Mateso unaoshangaza kwelikweli. Nami nina tumaini kwamba mpaka utakapofika mwisho wa mahubiri haya utasimama kwa heshima kuu na uchaji Mungu kutokana na mpango Wake wa ukombozi. Kwa hakika mimi yamenikuta hayo.

Lakini hiki ndicho kitu kinachoonekana hapa: Shetani hujaribu kuvuruga kila kitu kilicho muhimu kuhusiana na Maandiko. Bila kuchoka, Shetani anashambulia kila kitu kilicho muhimu katika biblia, akianza na Mwanzo sura ya 1. Na *mtiririko* wa matukio katika Wiki ya Mateso umekabiliwa na mashambulizi yasiyokoma kutoka kwa wasioamini. *Mtiririko* wa matukio umesababisha waumini wengi kutilia shaka kanuni ya kutokuwa na dosari katika Maandiko. *Mtiririko* wa matukio katika Wiki ya Mateso umesababisha wachungaji kama Dan Barker kutoka katika Imani na kuwa mkana-Mungu (atheist). Sasa, hata kwa dakika moja mimi sitakubaliana na hii dhana kwamba uwepo wa migongano ya kufikirika tu ndio ulimfanya aache imani yake. Kulikuwa na mengi yaliyokuwa yakiendelea ndani ya moyo wake mwovu zaidi ya kuona migongano katika Wiki ya Mateso. Alikuwa na matatizo ya kufikiri, lakini hili halikuwa tatizo lake moja pekee. Ila nilisumbuliwa na madai yake kwamba hakukuwa hata na mmoja kati ya wachungaji wake wa kiinjilisti ambao waliweza kujibu hoja za migongano inayoonekana kwa juu juu katika Wiki ya Mateso. Hili ni suala muhimu, na wainjilisti wengi wanatetereka juu yake. Hapa tunamwona mtoa-maoni mmoja wa kiinjilisti, John Wenham, akielezea suala hili:

> *Sasa, tunaona kwamba hadithi ya ufufuo wa Yesu inasimuliwa na waandishi watano tofauti, na masimulizi yao yanatofautiana kwa kiwango cha kushangaza sana.* [Huyu ni mwinjilisti anayeongea hapa, naye anasema "masimulizi ya Wiki ya Mateso yanatofautiana kwa kiwango kinachoshangaza sana."] *Imefikia kiasi kwamba wanazuoni wenye sifa mmoja baada ya mwingine wameeleza bila kujiuma-uma kwamba masimulizi haya kutoka kwa watu watano tofauti (pamoja na maelezo ya mtume Paulo) hayawezi kuoana. Tukirudi nyuma hadi karne iliyopita, yule mtoa-maoni maarufu mwenye msimamo mkali P. W. Schmiedel alisema: "Injili zote zinadhihirisha migongano mikubwa sana. Reimarus … aliorodhesha migongama ipatayo kumi; akini kiuhalisia kuna migongano zaidi ya hiyo." Hata yule mwinjilisti madhubuti asiyependa mabadiliko, Henry Alford, aliandika, "Katika mifumo yote ya matukio, <u>ile mifumo ya matukio</u> inayosimuliwa katika sura hizi kwangu mimi hairidhishi kabisa … inaonekana kudhoofisha ushahidi badala ya kuuimarisha … [mimi] nimeshakata tamaa kabisa juu ya dhana ya kuyaoanisha matukio yale."*[1]

Najua kwamba hii si namna nzuri wala ya kufurahisha ya kuanza mahubiri. Lakini mimi nimeridhika na kufurahishwa kabisa na mtiririko wa matukio katika Wiki ya Mateso ya Kristo. Nimesoma mapingamizi yote yanayosimulia migongano, na ninasema kwa kujiamini kabisa kwamba matukio yale yanaoana katika kila kipengele kwa namna inayorishisha kabisa.

Ebu tuanze kwa kuorodhesha nadharia tatu zinazoelezea siku ya kusulibiwa kwa Kristo. Kuna Nadharia ya kifo cha Bwana Yesu katika siku ya Jumatano, siku ya Alhamisi, na siku ya Ijumaa. Je, alikufa siku ya Jumatano, siku ya Alhamisi, au siku ya Ijumaa? Kama ukisoma masimulizi ya Injili moja tu ya kusulibiwa na kufa kwa Bwana wetu, basi nadharia ya kifo katika siku ya Ijumaa inaleta maana. Maandiko yanasema kwamba siku iliyofuata ilikuwa ni siku ya Sabato. Kwa kuwa Sabato ya Kiyahudi ya kila wiki ilikuwa katika siku ya Jumamosi, basi ikadhaniwa kwamba alisulibiwa katika siku ya Ijumaa, akabaki kaburini siku ya Jumamosi, na akafufuka siku ya Jumapili. Sasa mabishano yanatoka wapi? Kila kitu kinaonekana kana kwamba kimenyooka katika msitari mmoja, sivyo?

[1] John Wenham, *Easter Enigma*, (Paternoster Press. 1984), Introduction.

Katika miaka yote hii ya historia, wana-teolojia waliopambana kwa undani kabisa katika sehemu hii ya Maandiko, wamepasua vichwa vyao wakijaribu kupatanisha / kuoanisha siku ya kifo ya Ijumaa na dondoo nyingine nyingi zinazoorodheshwa katika Injili. Ukishikilia msimamo wa kusulibiwa kwa Bwana katika siku ya Ijumaa, basi hii itavuruga idadi ya siku ambazo Injili inazihesabu kutoka mwezi wa Nisan tarehe 10 mpaka siku ya ufufuo. Inavuruga pia tarehe ya Jumapili ya Matawi na kuifanya iwe Jumatatu ya Matawi, na hapo utalazimika kuchomeka siku ingine ya kufikirika ambayo Injili zote hazina habari nayo, na wale waliofanya hivyo wameshambuliwa na Wa-liberali kuwa wanaongeza maneno yao katika Maandiko (kitu ambacho ni dhambi) kutokana na kukwama katika hesabu na teolojia yao. Kama unashikilia msimamo wa tafsiri ya nadharia ya Ijumaa ambayo inadai kwamba Yesu alisulibiwa katika siku / tarehe ambayo kondoo wanachinjwa, yaani Nisan 14, basi hii inavuruga *mwaka* wa kifo Chake, na kuupeleka mwaka wa kifo Chake miaka kadhaa mbele au miaka kadhaa nyuma ya mwaka halisi. Kama unaamini kwamba alisulibiwa mwaka 30 BK, mwaka ambao wanazuoni wengi wanaamini ndio mwaka aliokufa (mimi huamini hivyo pia), basi hii inavuruga kabisa matukio mengine ya Wiki ile ikiwa utadai kwamba alikufa siku ya Ijumaa. Inavuruga umuhimu wa kinabii wa wakati wa kutenganisha kondoo [wa kafara], maonyesho mbele ya hekalu, na upako Wake. Lakini kama alikufa siku moja baadaye, katika tarehe ya Nisan 15 (kama ambavyo baadhi ya wanazuoni wapya wanavyodai ili kuoanisha baadhi ya aya na Nadharia ya Ijumaa), basi hiyo inafanya ule mlo wa Pasaka aliokula Bwana Yesu na wanafunzi Wake ulikuwa na nyama ya kondoo, kitu ambacho Injili zinakataa na kitu ambacho kinavuruga ibada ya Chakula cha Bwana, ambacho hakina nyama (ni mkate na divai). Pia tarehe hii inamfanya Kristo asiweze kutimiza unabii wa mtiririko wa matukio ya Pasaka ya kufa katika wakati wa kafara ya kondoo.

Sasa, ni lazima niseme hapa kwamba kuna maswali *mengine* ambayo Nadharia ya Ijumaa inayajibu kwa usahihi kabisa. Lakini wakati ninafanya uchunguzi na utafiti wa nadharia zote tatu ambazo kihistoria zimeshikiliwa na kanisa, kwa mara nyingine tena nilikutana na mpangilio na ulinganifu mzuri uliofanywa na Mungu, wa matukio yote ya Wiki ya Mateso, *ikiwa tu* tutasimama katika Nadharia ya Alhamisi katika mwaka 30 BK kama siku ya kusulibiwa na kufa kwa Bwana Yesu. Miaka kadhaa iliyopita, jarida la Time Life lilichapisha makala ambayo lengo lake lilikuwa ni kuonyesha kwamba mtiririko wa matukio ya Wiki ya Mateso ya Kristo hauwezekaniki. Lakini, hawa jamaa walikuwa wakishikilia msimamo wa Nadharia ya Ijumaa – hivyo hitimisho lao hili halinishangazi! Na kila moja katika migongano wanayoiorodhesha inayeyuka pale tu unaposimama katika Nadharia ya Alhamisi. Hivyo kutakuwa na dondoo mbili katika mahubiri yangu ya leo. Dondoo ya kwanza inajibu swali la ni siku ipi Bwana Yesu alisulibiwa na kufa, na dondoo ya pili inaainisha mpangilio na ulinganifu wa ajabu ikiwa utaelewa jibu sahihi la swali hilo la kwanza.

Sasa, somo hili si kwa ajili ya watu wavivu wa kufanya juhudi muhimu ya kufikiri. Haya ni mahubiri yanayotusaidia kwa mara nyingine tena kuuona utukufu mkuu katika ukweli kwamba Yesu aliienda kama ilivyotabiriwa katika unabii, na kwamba alipitia mateso yote katika siku zile kumi. Bwana Yesu alitimiza kwa utimilifu zaidi ya matukio 100 yaliyotabiriwa katika Agano la Kale, na alifanya hivyo katika namna ambayo imeupindua ulimwengu juu-chini. Lakini kama sitajadili kwanza suala la ni siku ipi alisulibiwa, utakosa sehemu kubwa ya utabiri huu uliotimia. Na hautakuwa na majibu ya kuwapa wakosoaji wa ki-liberali wala Wakristo wenzako wenye mashaka.

## I. Jinsi kusulibiwa, kufa na kuzikwa katika siku ya Alhamisi kunavyojibu “migongano” ambayo wa-liberali wanasisitiza kwamba imo katika masimulizi ya Wiki ya Mateso ya Bwana Yesu.

Ebu tuanze kwa kujaribu kueleza moja kati ya matatizo hayo. Wa-liberali wametoa mapingamisi yao kwa kusema kwamba aya za Matt. 27:63, Marko 8:31 na Yoh. 2:19 zote zinasema kwamba Kristo atakuwa kaburini kwa siku tatu, lakini tukiitazama Nadharia ya Ijumaa, Kristo alikuwa mfu kwa jumla ya masaa 39, na angekuwa kaburini kwa masaa machache zaidi ya hayo. Kutoka saa 9 alasiri, wakati wa kifo cha Kristo, mpaka saa 9 alasiri siku ya Jumamosi ni masaa 24. Saa 9 alasiri

Jumamosi mpaka saa 12 alfajiri katika siku ya Jumapili, ambayo ni saa ya mwisho kabisa inayowezekana kwa ajili ya ufufuo Wake ni masaa mengine 15. Wa-liberali wanatoa pingamizi kwamba masaa 39 ni machache sana ukilinganisha na masaa 72 (jumla ya siku 3), na wanakejeli. Wanasema kwamba Biblia ina makosa. Hakuwa kaburini kwa siku 3.

Kiuhalisia, pingamizi hili limejibiwa kwa kiasi fulani na kwa urahisi kabisa na wale wanaoshikilia mtazamo wa Nadharia [ya kale] ya Ijumaa. Nami wakati mwingine hufikiria hawa jamaa wa Nadharia za Jumatano na Alhamisi hawajawatendea haki wale wa mtazamo wa siku ya Ijumaa. Katika mfumo wa kuhesabu wa Kiyahudi, siku huhesabiwa "kwa pamoja", siku ya kwanza na ya mwisho zikihesabiwa, hata kama siku hizo hazikamilishi saa zote 24 zinazotakiwa kukamilisha siku moja. Hivyo katika kuhesabu siku tatu hakuna ulazima wa kuhesabu vipindi / vitambo 3 vyenye masaa 24 kila kipindi / kitambo, vikianza na siku Aliyozikwa, kama ambavyo Nadharia ya Jumatano inavyosisitiza. Yaani inaweza kumaanisha kitambo chochote cha muda kilichopitiwa au kilichoguswa na siku zote tatu. Kwa hiyo sehemu ya Ijumaa, Jumamosi yote na sehemu ya Jumapili zitahesabiwa kama siku tatu. Hivyo lile pingamizi la kwanza linakuwa si suala muhimu kabisa hapo. Nami nisingekuwa nahubiri juu ya jambo hili kama hilo lingekuwa pingamizi la pekee.

Lakini ukisoma Matt. 12:40, kunakuwa na suala moja la Maandiko ambalo haliwezi kujibiwa na Nadharia ya Ijumaa kuhusiana na siku hizo tatu. Sasa, nimetazama kila namna ya kutetea Nadharia ya Ijumaa, na sikuweza kupata namna yoyote. Katika Matt. 12:40, Yesu anasema, “Maana kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi; vivyo hivyo Mwana wa Adamu atakuwa ***siku tatu mchana na usiku*** katika moyo wa nchi”. Hii ni tofauti na kusema tu “siku tatu.” Pana ulazima wa kuwako angalau sehemu ya mchana na sehemu ya usiku katika usiku na mchana wa siku zote tatu. Kwa kuwa Yoh. 20:1 inatutaarifu kwamba Yesu aliinuka wakati kukiwa bado na giza katika siku ya Jumapili, hii ina maana kwamba katika Nadharia ya Ijumaa, Yesu alikuwa kaburini kwa saa chache za mchana wa Ijumaa na mchana wote wa Jumamosi (hivyo kufikisha siku mbili za mchana), na alikuwa kaburini usiku wa Ijumaa na usiku wa Jumamosi (na kutimiza siku mbili za usiku). Hivyo hata ukihesabu kwa “mfumo wa pamoja,” unapata tu siku mbili (mchana) na siku mbili (usiku).

Acha sasa nieleze tofauti kati ya “kuhesabu siku kwa pamoja - inclusively” na “kuhesabu siku kwa utenganisho - exclusively). Nitatumia analojia. Ikiwa nguzo za uzio wa eneo fulani zinasimikwa kila baada ya futi 20 za barabara ya futi 1000, utahitaji nguzo ngapi? Ukigawanya 1000 kwa 20 utapata 50, lakini ukinunua nguzo 50 tu, utapungukiwa na nguzo 1, kwa sababu ni lazima usimike nguzo 1 katika kila ncha, yaani mwanzo na mwisho wa barabara. Hivyo utahitaji nguzo 51. Huu ndio mfumo wa kuhesabu “kwa pamoja,” na kwa hakika tunafanya hivyo mara nyingi tu katika maisha yetu. Hakuna kitu cha kushangaza hapo kabisa. Katika kalenda unaweza kuhesabu “kwa pamoja” au “kwa utenganisho.” Unaweza kuihesabu siku ya mwanzo au unaweza kuiacha. Hii ni kweli katika siku za kale na katika siku hizi. Katika siku ya Jumapili ninaweza kusema, “Nitasafiri katika siku mbili,” nawe yumkini utafikiria “Jumanne.” Huo, sasa, ni mfumo wa kuhesabu “kwa utenganisho.” Njia zote mbili za kuhesabu ni halali. Na jambo ninalotaka kusema hapa ni hili: karibu yote yanayoitwa “makosa” ambayo watu wanayazungumzia ni tofauti tu kati ya ‘kuhesabu kwa pamoja’ na ‘kuhesabu kwa utenganisho.’ Si kwamba njia moja ni sahihi na nyingine si sahihi. Zote mbili ni njia za kuhesabu kitu kile kile. Na kama unahitaji taarifa zaidi juu ya hili, unaweza kwenda katika tovuti ya Wikipedia na kusoma “inclusive counting” na utaona mifano kadhaa ya jinsi tunavyotumia njia zote mbili katika kuhesabu kila siku, na tunazichukulia zote kuwa halali na sahihi.

Hivyo katika Nadharia ya Jumatano, wanajaribu kumjibu m-liberali kwa kusema kwamba Yesu alisulibiwa siku ya Jumatano na alikuwa katika kaburi siku tatu za masaa 24 [kamili], hesabu yake ikifikia saa 72. Lakini wanajikuta wakilazimika kusema Yesu alifufuka Jumamosi badala ya Jumapili! Ila ukiacha doa hili, kuna kiasi fulani cha mantiki katika msimamo wao huu. Wanatumia

mfumo wa ‘kuhesabu kwa utengano’. Hii ni halali, *ikiwa* Maandiko yanatulazimu kufanya hivyo. Lakini kwa bahati mbaya, mtazamo huu unaleta matatizo mapya, kama ambavyo majedwali nitakayoonyesha hapa chini yatakavyoonyesha. Katika majedwali haya, utaona kwamba katika vipimo 20 nilivyotumia kutathmini Nadharia hizi tatu, Nadharia ya Jumatano inapata alama 9 kati ya 20. Lakini hii ni bora Zaidi ya Nadharia ya Ijumaa, ambayo inapata alama 6 kati ya 20. Sisi tunataka kupata nadharia itakayotupatia 20/20. Ebu tuanze kuchambua namna nadharia hizi zinavyopata alama za ushindi katika Ubao wa Alama.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Yesu alikuwa “siku tatu *mchana* na siku tatu *usiku* katika moyo wa nchi” (Matt. 12:40), siyo tu siku mbili mchana na siku mbili usiku (kama ilivyo katika Nadharia ya Ijumaa). | √ | √ | X |

Je, Nadharia ya Alhamisi inaoana vipi na Ubao wa Alama namba 1? Bwana Yesu alizikwa *kabla ya sabato kuanza* (soma Yoh. 19:31). Katika Uyahudi, *siku ilianza saa 12 jioni*. Hii inamaanisha mwili wa Bwana wetu ulikuwa kaburini kabla ya mchana wa Alhamisi kuisha; hivyo tukihesabu ‘kwa pamoja’, Alhamisi ile inahesabiwa kama siku ya kwanza. Katika Kiingereza Matt. 12:40 inasomeka vizuri zaidi, “3 days and 3 nights” (KJB), tofauti na Kiswahili – “siku 3 mchana na siku 3 usiku” (“siku 3 mchana na usiku” - SUV). Kutokana na mpangilio wa siku za sabato, kulikuwa na vipindi / matokeo matatu ya wakati wa mchana na wakati wa usiku katika mwaka 30 BK yaliyooana na kifo cha Bwana wetu katika siku ya Alhamisi. Tofauti na ilivyo katika Nadharia ya Ijumaa ambapo Yesu alikuwa kaburini kwa sehemu tu za siku mbili mchana na usiku, katika Nadharia ya Alhamisi, Alikuwa kaburini kwa siku tatu, mchana na usiku.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Mfuatano ni wa mchana kwenda usiku, na si usiku kwenda mchana (Matt. 12:40).[2] | X | √ | √ |

Lakini tukirejea kwenye Ubao wetu wa Alama, je, unakidhi kigezo chetu cha pili ambacho ni *mfuatano* wa siku, mfuatano huo ukiwa ni *mchana* kwenda usiku kwa siku tatu, na *si usiku* kwenda mchana? Jibu ni ndiyo. Mwili wa Yesu uliwekwa kaburini kabla ya Sabato kuanza, wakati mwanga wa jua ukingali unaangaza. Aliwekwa kaburini katika wakati wa mchana, yaani kabla ya saa 12 jioni. Lakini Maandiko hapa yanasema juu ya *nafsi* ya Yesu kuwa katika moyo wa dunia – katika Sheol. Tukio hili [la kuingia Sheol] lilianza saa 9 alasiri siku ya Alhamisi. Lakini vyovyote vile utakavyotafsiri suala hili, kifo Chake na maziko Yake yalikuwa wakati wa saa za mchana za siku ya Alhamisi. Tofautisha hii na Nadharia ya Jumatano, ambayo inasisitiza kwamba Yesu aliwekwa kaburini baada ya giza-giza kuingia, na baada ya Sabato kuanza – yaani baada ya saa 12 jioni. Hivyo mfuatano wao ni usiku-mchana na si mchana-usiku (*siku tatu usiku na mchana*). Hii ni dondoo ndogo tu, lakini kwa sababu wanajisifu kwamba nadharia yao ina usahihi mpaka katika *saa* ya kila tukio, tunahitaji kudhihirisha kwamba hii si kweli. Nami naamini kwamba katika suala hili, kama katika masuala yote muhimu, tunapaswa kuwa sahihi mpaka katika *saa ya tukio*.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Hesabu yetu inapaswa kuoana na ukweli kwamba Yesu alisema kuwa Yeye “atauawa, na *baada* ya siku tatu, atainuka” (Mar 8:31; cf. Matt. 27:63)[3] | X | √ | X |

Dondoo ya tatu katika Ubao wetu wa Alama ni kwamba Marko 8:31 inasema kuwa Yesu “atauawa, na *baada* ya siku tatu, atainuka tena.” Neno hili “baada” linaleta tatizo kubwa sana kwa nadharia

……………………

[2] Nadharia ya Jumatano inaanza hesabu yake baada ya saa 12 jioni tarehe 14 mwezi wa Nisan, hivyo hesabu yao inaanza na usiku.

[3] Kwa kuwa Nadharia ya Jumatano inaukataa mfumo wa “kuhesabu kwa pamoja”, hawawezi kueleza maana ya aya hii. Hata hivyo, licha ya kutumia mfumo huu wa kuhesabu, Nadharia ya Ijumaa (soma dondoo inayofuata), haiwezi kueleza maana ya aya hii pia.

zote mbili, ya Jumatano na ya Ijumaa. Msingi pekee wa Nadharia ya Jumatano ni mfumo wa kuhesabui wa utenganisho. Kwa hakika, hakuna sababu ya kuiamini Nadharia ya Jumatano ikiwa hutashikilia msimamo kwamba utahesabu siku hizo kwa mfumo wa utenganisho *pekee*. Neno *baada* pia linafuta uhalali wa Nadharia ya Ijumaa, ambayo kwa wazi kabisa haiwezi kutetea kwa ufanisi hoja ya ufufuo wa *baada* ya siku tatu, mchana na usiku, kwa *mfumo wowote* ule wa kuhesabu, uwe wa pamoja au wa utenganisho. Wanajaribu kulifanya neno "baada" liwe linamaanisha baada ya kukamatwa na kuhojiwa katika mahakama ile batili, lakini Maandiko yako wazi kwamba yanahesabu kutoka *kifo* cha Yesu, na si kuhojiwa Kwake. Kama Yesu alizikwa jioni ya Ijumaa, basi Jumapili haiwezi kuwa baada ya siku tatu hata ukiinyumbulisha namna gani. Lakini katika Nadharia ya Alhamisi, Jumapili inakuwa ni baada ya siku tatu. Una Alhamisi, Ijumaa, na Jumamosi na baada ya siku hiyo inakuja Jumapili. Ni mfumo sahihi kabisa wa kuhesabu.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Virai (misemo) kama hivi: "baada ya siku tatu" (Marko 8:31; cf. Matt. 27:63), "baada ya siku mbili … ikifika siku ya tatu" (Hosea 6:2 – tazama 1Wakor. 15:4), "katika siku tatu" (Matt. 20:61; Marko 15:29; Yoh. 2:19), "ndani ya – katika - siku tatu" (Marko 14:58), "siku ya tatu" (Matt. 16:21; 17:23; 20:19; Marko 9:31; 10:34; Luka 9:22; 13:32; 18:33; 24:7; 24:46; 1Wakor. 15:4), na "katika siku ya tatu" (Matendo 10:40) vinaonyesha kwamba mifumo yote miwili ya kuhesabu, mfumo wa pamoja na ule wa utenganisho, inatumika katika Biblia kama inavyotumika katika siku za leo.[4] | X | √ | X |

Lakini ebu tuendelee. Wa-liberali wanaleta pingamizi kwamba aya moja inasema Aliinuliwa "katika – ndani ya – siku tatu" na nyingine inasema Aliinuliwa "baada ya siku tatu." Oh ooooh! Wanasema huwezi ukatumia namna zote mbili za kuhesabu. Ni lazima iwe "ndani ya" au "baada ya," siku tatu; ki-mantiki huwezi ukawa na matumizi yote mawili kwa wakati mmoja. Wanafikiri huu ni mgongano wa wazi. Kwa hakika, ukitazama juu-juu tu, unaonekana kuwa ni mgongano. Lakini mimi nitasema kwamba kuna maswali mawili ambayo wa-liberali hawa wanapaswa kuyauliza juu ya Maandiko. Swali la kwanza ni je, inawezekana Marko anaweza kujiingiza mwenyewe katika mgongano wa ki-mantiki ndani ya aya 37? Uwezekano wa hili kutokea ni mdogo sana. Na swali la pili ambalo ni muhimu sana kulielewa ni, "Mwandishi alikuwa anaelekeza maandiko yake kwa wasomaji gani? Wasomaji wake walikuwa ni Wayahudi au watu wa Mataifa?"

Ukitazama waandishi ni nani na wasomaji ni nani, basi unapata jibu harakat u. Marko *mwenyewe* anasema "baada ya siku tatu" katika Marko 8:31, lakini kwa usahihi kabisa anamnukuu *Yesu* akisema "atafufuka siku ya tatu" katika Marko 9:31. Watu wawili tofauti wanazungumza na wasikilizaji tofauti. Yesu alikuwa akizungumza na Wayahudi waliokuwa na desturi ya kuhesabu kwa pamoja, na Marko alikuwa akieleza maana ya maneno ya Yesu kwa Warumi waliokuwa na desturi ya kuhesabu kwa utenganisho. Lakini pia Marko hakuwa anaeleza kwa kubadilisha maneno ya Kristo. Hii ingesababisha dosari katika Maandiko. Badala yake, ingawa maneno yake yangeweza kuwashangaza wasomaji wake wa Kirumi, Marko ananukuu maneno ya Yesu kama alivyoyatamka

………………………………………

[4] Ni kawaida kwa watetezi wa Nadharia ya Jumatano kusisitiza kwamba masaa 72 ni lazima yakamilike ndani ya kaburi, wakitoa hoja kwamba Biblia siku zote inatumia "mfumo wa kuhesabu kwa utenganisho." Watetezi wa Nadharia ya Ijumaa nao wanasimama katika kauli kwamba mfumo unaotumika katika Biblia ni ule "wa pamoja." Lakini ni wazi kabisa kwamba Wayahudi wamekuwa wakitumia mifumo yote miwili kama ambavyo watu wa nchi za Magharibi na kwingineko leo hii wanafanya. Tafakari juu ya mifano ifuatayo ya kuhesabu kwa utenganisho: Mwanzo 1; Yoh. 2:19. Au tafakari juu ya mifano hii ya kuhesabu kwa pamoja: Luka 13:32-33; 2Wafa. 18:9-10; 1Wafa. 22:1-2, 29-31.

Mwenyewe, na anatafsiri kilichomaanishwa, kwa wasomaji wa Mataifa. Maandiko hayana hitilafu! Huu ni usahihi usiopimika wa Maandiko. Marko anataka kumnukuu Bwana wetu bila makosa, na anataka kuwasilisha ujumbe wa Yesu bila makosa kwa wasomaji wake.

Nadharia za Jumatano na Ijumaa zote zinashindwa kujitetea kwa kutoa maelezo ya namna hizi mbili za kufasili matukio. Si kwamba ni mgogoro unaoonekana machoni mwa msomaji tu, kwa juu-juu tu, bali ni mgogoro halisi uliopo katika nadharia zote mbili, ya Jumatano na ya Ijumaa. Na tatizo la nadharia zote mbili ni kwamba zinasisitiza kwamba Maandiko yana mfumo mmoja tu wa kuhesabu kati ya mifumo miwili – kuhesabu kwa utenganisho au kuhesabu kwa pamoja. Nami nauliza – kwa nini iwe hivyo? Kwa nini mtu ajiamulie tu kusema hivyo? Wanashindwa kufikiria kwamba injili hizi mbalimbali ziliandikwa kwa wasomaji tofauti, walengwa tofauti. Nadharia kadhaa za Ijumaa zimesisitiza kwamba mfumo wa kuhesabu kwa pamoja ni wa Kiyahudi na mfumo wa kuhesabu kwa utenganisho ni wa nchi za Magharibi pekee. Na katika ujumla wake hii ni kweli. Lakini katika kielelezo cha nguzo za uzio hapo juu nilidhihirisha kwamba watu wa nchi za Magharibi wanatumia mfumo wa kuhesabu wa pamoja mara nyingi tu. Kwa upande mwingine, nilisoma makala ya mtetezi mmoja wa Nadharia ya Jumatano akisema, "Sikumbuki hata mfano mmoja wa mfumo wa kuhesabu kwa pamoja katika Maandiko." Lakini hii ni kauli ya kuchekesha. Kila Fasiri ya Biblia niliyo nayo inasema kwamba Luka 13:32 ni mfano timilifu wa mfumo wa kuhesabu kwa pamoja. Yesu anasema, "**Tazama, nafukuza pepo na ninaponya watu leo na kesho, na [*siku*] ya tatu nitatimilishwa**". Kuhesabu Kwake kunaihusisha *siku ya leo* kwa dhahiri kabisa. Unapoihusisha "siku ya leo" katika hesabu yako, basi hapo unatumia mfumo wa kuhesabu kwa pamoja. Sasa unaanza kuelewa?

Mifumo yote miwili ya kuhesabu ilitumiwa katia Agano la Kale na Jipya, kama ambavyo mifumo yote miwili inatumika katika maisha yetu ya kila siku, kila mahala hapa duniani, leo hii. Lakini Waebrania / Wayahudi walikuwa na desturi ya kutumia na kutafsiri matukio kwa mfumo wa pamoja unapozungumza nao (na Nadharia za Alhamisi na Ijumaa zinategemea hivyo), wakati Warumi walikuwa na desturi ya kutumia na kutafsiri matukio kwa mfumo wa utenganisho (na Nadharia ya Jumatano inategemea hilo, ila inautumia kupita kiasi). Hivyo, hitimisho la mjadala huu ni kwamba tunapaswa kuelewa kwamba Marko alijieleza kwa usahihi kabisa wakati ananukuu maneno ya Yesu (yaliyotolewa katika mfumo wa kuhesabu kwa pamoja wakati anazungumza na Waebrania) wakati anaandika kwa wasomaji wa Kirumi katika mfumo wa kuhesamo kwa utenganisho. Si Myahudi wala Mrumi angekanganyikiwa kwa matumizi ya mifumo yote miwili. Lakini ukichukua mtazamo [usio sahihi] kwamba mifumo hii miwili ina mgongano, basi hautoweza kuoanisha misemo au virai nilivyoorodhesha katika majedwali hapa. Kwa kiasi kikubwa lugha inayotumika ni ya mfumo wa kuhesabu kwa pamoja, lakini lilikuwa jambo la msingi kwa Marko na Luka kuandika katika mfumo wa kuhesabu kwa utenganisho kwa sababu wao waliandika kwa wasomaji wa Mataifa.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Kristo alitimiza kalenda ya kinabii ambayo ilijumuisha mlo wa Pasaka usiokuwa na nyama mwanzoni mwa mwezi wa Nisan, tarehe 14 (Kutoka 12:18 pamoja na Marko 14:12; Luka 22:7), kuchinjwa kwa kondoo kabla ya mwisho wa siku ya Nisan 14 (Hesabu 28:16; 2Mambo ya Nyakati 30:15; 35:1 pamoja na Marko 14:12; Luka 22:7) na kondoo wa Pasaka waliopangwa kuliwa na Wayahudi wengine mwanzoni mwa tarehe 15 ya mwezi wa Nisan (Hesabu 28:17; tazama Yohana 13:1-2).[5] Kama hakuna tukio la kifo cha Kristo katika Nisan 14, ni vigumu kuona kutimizwa kwa kalenda ya kinabii (isipokuwa tukio la dhabihu pekee). | √ | √ | X |

[5] Ukikumbuka kuwa kuna aya nyingi zinazotuambia kwamba Kristo ni sadaka yetu ya Pasaka, na kila kipengele cha kalenda ya unabii kikikaa mahala pake, inakuwa ngumu kuelewa kwa nini Nadharia ya Ijumaa inasisitiza kwamba Yesu hakusulibiwa tarehe 14 mwezi wa Nisan, bali alisulibiwa siku ya Karamu ya Sabato, Nisan 15 (ambayo ni tofauti na Sabato ya Jumamosi). Yoh. 13:1-2 na 19:14 ni aya zinazotulazimisha tuhitimishe kwamba chakula cha mwisho jioni ile kilikuwa Nisan 14 (katika mwaka 30 BK hii ilikuwa Jumatano jioni) na hivyo msalaba ulikuwa Nisan 15 (katika mwaka 30 BK, hii ni Alhamisi).

Dondoo ya tano ni kwamba Nadharia ya Ijumaa inatibua sehemu kubwa sana ya kalenda ya unabii. Hii haikuwa hivyo hapo zamani. Na hii ni kwa sababu wanazuoni hawakuwa na ufahamu wa maana na matokeo (implications) za baadhi ya tarehe husika. Lakini Edersheim alijaribu kuiokoa Nadharia ya Ijumaa kwa kupendekeza kwamba Yesu alisulibiwa mwaka 34 BK. Na tukiunganisha na ukweli kwamba hakuwa na kompyuta ya kukokotoa mizunguko yote ya mwezi kwenda tarehe za nyuma hadi kufika karne ya kwanza, ni jambo la kumpongeza sana kwamba alikosea kwa siku moja tu! Alikuwa ni mtu mwenye akili sana! Alikuwa mwanazuoni wa kiwango cha juu kabisa. Lakini siku [hiyo] moja inavuruga kila kitu. Na kila mtu aliyetumia programu ya kalenda ya kompyuta anakubaliana kwamba alikosea kwa siku moja. Alikosea. Hivyo, kama unataka kumtumia Edersheim kuitetea Nadharia ya Ijumaa, taarifa zako zimepitwa na wakati.

Mara programu za kalenda za kukokotoa mizunguko ya mwezi zilipoanza kutumika kuanzia mwaka 1973 na kuendelea, kila mtu alijua Edersheim alikosea, na mwaka 34 BK hauwezi kuwa ndio mwaka wa kifo cha Bwana wetu. Kuna matatizo mengine mengi katika tarehe za miaka ya 33 BK na 34 BK pia, hivyo idadi kubwa ya wanazuoni wamejiridhisha kwamba Yesu alikufa mwaka 30 BK, hata kama tarehe hiyo ina matatizo kiasi gani. Nami pia nashika msimamo huo huo wa mwaka 30 BK. Nafikiri hii ni tarehe sahihi. Hali hii ilisababisha mabadiliko mengi katika fikra kuhusiana na suala hili, nami pia nililazimika kusoma Makala nyingi zinazotetea Nadharia ya Ijumaa. Wengi kati ya waandishi wa Nadharia ya Ijumaa wamelazimika kuiacha tarehe 14 Nisan kama tarehe ya kifo cha Yesu. Kwa ujumla tarehe hii haiwezekaniki. Badala yake, wanasema kwamba Alisulibiwa siku inayofuata. Lakini katika kutatua tatizo moja, wanakutana na matatizo mengine.

Moja kati ya matatizo hayo ni kwamba Nisan 15, siku / tarehe ambayo sasa wanasema ndiyo Alisulibiwa, ni Sabato kuu, moja kati ya Sabato muhimu sana katika mwaka mzima. Na kushiriki katika kumsulibisha mtu [yeyote] katika siku hii ya Sabato kuu ni jambo lisilowezekana kabisa kwa Wayahudi wale wafuata-sheria kulifanya. Ebu twende kusoma Yohana 19. Katika aya ya 31, tunasoma, "**Basi Wayahudi, kwa kuwa ilikuwa ni Siku ya Maandalizi, na ili miili isikae juu va msalaba siku ya Sabato (maana siku ile ilikuwa Sabato kuu),** [anaeleza kwamba hii haikuwa Sabato ya kawaida …] **wakamwomba Pilato, miguu yao ivunjwe, ili waondolewe**. Kitu muhimu cha kuona hapa ni kwamba Wayahudi hawa waliokuwa wafuataji wa sheria hawakutaka wahanga wao wale watatu wabaki katika misalaba yao katika siku ya Sabato. Na bado watetezi wa Nadharia ya Ijumaa wanataka [sisi] tukubali kwamba Wayahudi hawa walikuwa wanaizungumzia Sabato *ya kila wiki* ambayo ni siku ya Jumamosi, na kwamba hawakuwa na tatizo katika kufanya kazi siku ya Sabato ya *Pasaka* ambayo ilikuwa Ijumaa katika mwaka ule wa 30 BK. Haiwezekani kabisa kwa Wayahudi wale kufanya mambo kama yale katika siku ya Sabato ya Pasaka. Sabato ni Sabato; ni siku kuu; haiwezekani kabisa kufanya mambo waliyokuwa wakimfanyia Yesu katika siku ya Sabato.

Na hata kama ingekuwa sawa kwa wao kufanya kazi hiyo yote katika siku ya Sabato ya Pasaka, bado hakiendani na aya za maandiko katika sura ya 19. Tazama aya ya 42: "**Humo basi, kwa sababu ya siku ya Maandalizi ya Wayahudi, wakamweka Yesu; maana lile kaburi lilikuwa karibu**." Walikuwa na haraka sana. Hawakuwa na muda wa kufanya zaidi ya yale waliyoweza kwa sababu Sabato ilikuwa karibu kuanza. Lakini watetezi wa leo wa Nadharia ya Ijumaa ambao bado wanataka kuiokoa nadharia yao na kuendelea kuiweka katika mwaka 30 BK wanasisitiza kwamba siku ile ilikuwa ni Sabato ya wiki, na si Sabato ya Karamu / Sherehe iliyokaribia. Lakini haikuwa hivyo. Yohana alikwishabainisha ni Siku gani ya Maandalizi aliyokuwa anaizungumzia. Tazama aya ya 14: "**Ilikuwa ni siku ya Maandalizi ya Pasaka**." Hii si Siku ya Maandalizi kwa ajili ya Sabato ya wiki. Hii ilikuwa Siku ya Maandalizi kwa ajili ya Sabato ya Pasaka, ambayo ilikuwa ni moja kati ya Sabato 7 za mwaka mzima. Na kama tulivyoona, aya ya 31 inaitambua siku hii kuwa ni Sabato kuu. Haiwezekani kabisa kwamba walifanya kazi hii katika siku ya Sabato kuu.

Hivyo siku baada ya kusulibiwa Kristo ilikuwa ni Nisan 15. Hapo Nadharia ya Ijumaa inabomolewa kabisa. Ukitazama kalenda ya Kiyahudi ya mwaka 30 BK, utaona kwamba Nisan 14 ilikuwa

Alhamisi, Nisan 15 ilikuwa Ijumaa, na Nisan 16 ilikuwa Jumamosi. Yuda asingeweza hata kufikiria kwenda kununua vitu (Yoh. 13:29) katika siku ya Sabato (tazama Ubao wa Alama #8). Hivyo vitu angevinunua wapi?! Kila duka, soko lingekuwa limefungwa. Katika Israeli ya kale ilikuwa ni kinyume cha sheria kufungua duka na soko katika siku zote za Sabato. Vivyo hivyo, ilikuwa haiwezekani kwa Nikodemo kununua sanda katika siku ya Sabato (tarehe 15 Nisan), na hata asingeweza kumpata mtu yeyote wa kumwuzia sanda hiyo. (Hii iko katika Ubao wa Alama #9). Ukikosea kwa siku moja, basi inakuwa kama mchezo wa domino / dadu, kila kitu kinavurugika.

Suala jingine muhimu la kukumbuka ni kwamba Matthayo na Marko wote wanataja zaidi ya siku moja ya Sabato kabla ya Jumapili. Hili ni jambo la kuvutia sana. Lakini hakuna Injili hata moja inayotaja zaidi ya siku moja ya Maandalizi. Umeiona hiyo? Kuna siku moja tu ya Maandalizi lakini kuna Sabato zaidi ya moja. Hii ina maana kwamba Sabato hizi zilifuatana – mf. leo na Kesho, na hii ilitokea katika mwaka 30 BK pekee. Katika mwaka 30 BK Ijumaa ilikuwa Sabato kuu ya Pasaka na Jumamosi ilikuwa Sabato ya wiki. Hivyo siku ya Maandalizi ilikuwa Alhamisi.

Yohana anaweka bayana kwamba Kristo alisulibiwa katika siku ya Maandalizi ya Pasaka. Hivyo dondoo #7 ni hoja dhidi ya Nadharia ya Jumatano pia, kwa kuwa hakuna ushahidi kwamba kulikuwa na siku mbili za Maandalizi – moja Jumatano na nyingine Ijumaa. Kama Nadharia ya Jumatano ingekuwa sahihi (na kama Angesulibiwa mwaka tofauti na 30 BK) basi Jumatano na Ijumaa zingeitwa siku za Maandalizi. Hii inatupatia ushahidi wa nguvu kwamba Sabato hizi mbili hazikutenganishwa na siku moja ya Ijumaa ambayo haikuwa Sabato, bali ni Sabato zilizofuatana – yaani leo na kesho. Na kwa hakika katika mwaka 30 BK Sabato hizi mbili zilifuatana. Ijumaa tarehe 15 Nisan ilikuwa Sabato Kuu, halafu Jumamosi ilikuwa ni Sabato ya kawaida ya wiki. Na hivyo utahitaji siku moja tu ya Maandalizi kwa ajili ya Sabato zote mbili – ambazo zinafuatana. Marehemu James Montgomery Boyce anazizungumzia Sabato hizi namna hii:

> “Masimulizi ya Matthayo kuhusiana na matukio ya asubuhi ya siku ya Ufufuo yanaanza, ‘Baada ya Sabato zile (wingi) kwisha, alfajiri ilipoanza kuelekea siku ya kwanza ya wiki’ (Matt. 28:1). Neno Sabato lililo katika uwingi (plural) limewatia bumbuwazi waandishi wengi watoa-maoni na wafasiri wa Biblia, ambao hubadilisha uwingi na kuweka neno Sabato katika umoja (singular). Lakini ‘Sabato’ katika uwingi inaeleweka kwa ukamilifu ikiwa kulikuwa na Sabato mbili katika wiki ile, Sabato ya Pasaka ya siku ya Ijumaa na Sabato ya Jumamosi, zilizofuatana.”

Sasa acha nianze kuimaliza sehemu hii ya kwanza. Kama Nadharia ya Alhamisi ni sahihi, basi inaleta tofauti kubwa sana. Inamaanisha kwamba Yesu alishiriki katika mlo wa Pasaka ya kwanza tarehe 14 Nisan, na si mlo wa nyama ya kondoo wa Pasaka tarehe 15 Nisan. Hapa naona tunarudi tena kwenye dondoo #5 ya Ubao wetu wa Alama. Kama Yesu alikula mlo wa Pasaka jioni ya Jumatano, mwanzo wa Nisan 14 (nami naamini hivyo), basi *mlo ule haukuwa na nyama*. Mlo wote ulikuwa sherehe iliyohusisha mkate na divai. Kondoo wanachinjwa saa nane baadaye siku hiyo hiyo - Nisan 14, halafu nyama ya kondoo ingeliwa mwanzoni mwa Nisan 15 jioni Alhamisi. Mkate na divai vilikuwa mlo katika siku zote mbili, lakini katika Sabato ya Pasaka (ile Sabato ya pili ya wiki ile) ya Nisan 15, msisitizo ni kondoo na siyo mkate. Kama tutakavyoona punde tu, Yesu aliasisi Chakula cha Bwana kilichokuwa na mkate na divai *pekee* kwa sababu siku iliyofuata Yeye ndiye atakuwa Kondoo *wa mwisho* kutolewa dhabihu. Hakutaka ushindani, na kwa hakika Hakutaka kuasisi damu na nyama kwa ajili ya Meza ya Bwana milele. Kuanzia pale na kuendelea, mkate umekuwa *ishara* tu ya mwili / nyama, na divai ni *ishara* ya damu, kama ambavyo ubatizo wa maji umechukua nafasi ya tohara. Hakuna tena dhabihu [nyingine] baada ya dhabihu ya Yesu kukamilika.

Hapa kuna mambo mengine yatakayovurugika ikiwa utapuuza matatizo ya mwaka 26 BK au 33 BK (nayo ni mengi na makubwa) na ukadai kwamba Yesu alisulibiwa tarehe 14 Nisan. Kwanza, utakuwa na Jumatatu ya Matawi badala ya Jumapili ya Matawi (hivyo utakuwa umeachana na

mapokeo, vyovyote utakavyolitazama jambo hili) na inavuruga kabisa mpangilio wa wiki ile. Na sababu pekee ninataja mapokeo hapa ni kwa sababu [mapokeo] ndiyo hoja kuu ya watetezi wa Nadharia ya Ijumaa. Lakini tatizo liko hapa - ikiwa utatazama sehemu ya mwisho ya chati iliyoko katika ukurasa wa sita, utaona kwamba hakuna hata nadharia moja kati ya nadharia hizi tatu inayosapoti mapokeo ya [desturi ya kuhesabu ya] Magharibi. Hakuna nadharia inayofanya hivyo. Hivyo hii si hoja yenye nguvu.

Lakini kuna tatizo jingine katika hii nadharia mpya zaidi, [tuseme ‘ya kisasa’] ya Ijumaa. Utaona kwamba Yesu hafi katika wakati ambao kondoo wanachinjwa. Bado hakai kaburini kwa siku tatu ‘usiku na mchana’. Na kuna matatizo mengine tena katika nadharia za Ijumaa na Jumatano. Katika tarehe za 26 BK na 33 BK, kondoo wanachinjwa saa mbili *kabla* ya kuuawa kwa Bwana Yesu, na giza linachelewa kwa saa mbili na hivyo linasitisha matayarisho ya dhabihu hekaluni. Ni tukio la kipekee kabisa kwamba Sabato zilifuatana katika mwaka 30 BK – Ijumaa na Jumamosi – na ni kwa sababu hiyo pekee ndiyo dhabihu ilifanyika saa 9 alasiri badala ya saa 7 mchana.

Na kuna mkusanyiko mkubwa sana wa ushahidi ambao asubuhi ya leo sitauzungumzia unaodhihirisha kwamba Alhamisi inaoana na mpangilio wa Uasisi wa Agano Jipya, wa kalenda mpya, na unaweka mwelekeo wa fikra zetu kwa Yesu katika namna ya kipekee kabisa kiasi kwamba mimi ninaweza kutabiri kwamba katika miongo kadhaa ijayo wengi kati ya wanazuoni wa kiinjilisti watakubaliana na Nadharia ya Alhamisi. Kuna idadi kubwa tu ambao wameshakubaliana nayo, na kuna wengine kadhaa ambao hawana uhakika na nini wanachokiamini, lakini wanasema kwamba tunapaswa kuirejesha tena Alhamisi katika meza ya majadiliano. Hata watetezi wa mwanzo wa Ijumaa kama Ernest Martin wamebadilika na kuikumbatia Nadharia ya Alhamisi. Nadharia ya Alhamisi inaleta maana kabisa. Sitakusumbua na zile dondoo nyingine 14, lakini hizo zinajenga hoja kwa utaratibu mzuri hadi kufikia hitimisho kwamba Alhamisi ndiyo ilikuwa siku Bwana Yesu alisulibiwa. Nilitaka chati ikamilike zaidi kwa ajili ya mafaili yenu. Lakini ebu tuendelee na kutazama mpngilio adhimu wa Mungu wa matukio ya Wiki ya Mateso kama Alivyokusudia. Kuna ulinganifu usiomithilika kama utashikilia Nadharia ya Alhamisi. Nami nakumbuka nilitoa baadhi ya dondoo hizi miaka kadhaa iliyopita.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6 | Tukio la msalaba linafanyika kabla ya ‘siku ya Sabato *ya Karamu*’ (Yoh. 19:14 – “Siku ya Maandalizi *ya Pasaka*”), ambao ni ushahidi wa ziada kwamba tukio lilikuwa tarehe 14 Nisan. Aya za Walawi 23:5-7; Hesabu 28:7-18; nk zinaonyesha kwamba Nisan 15 ilikuwa ndiyo siku hii ya Sabato ya Karamu. | √ | √ | X |
| 7 | Kuna siku moja tu “ya Maandalizi” inayotajwa katika Injili zote nne – Siku ya Maandalizi ya Pasaka (Yoh. 19:14). Katika mwaka 30 BK siku hii ya maandalizi inaangukia katika tarehe 14 mwezi wa Nisan na si Nisan 15 kwa sababu Sabato zilifuatana (Ijumaa na Jumamosi). Katika Nadharia ya Jumatano tungetarajia siku mbili tofauti (Jumatano na Ijumaa). | | | |
| 8 | Hoja ya kwamba Yesu alikula mlo wa mwisho mwanzoni mwa Nisan 14 badala ya mwanzoni mwa Nisan 15 inatiwa nguzu zaidi na ukweli kwamba Yohana 13:29 inaashiria uwezekano wa kununua vitu katika siku hiyo. Hii inawakilisha mapigo mawili dhidi ya [Nadharia ya] Ijumaa: 1) karamu inayokuja itakuwa ni matayarisho ya mlo wa nyama ya kondoo wa Nisan 15, na 2) Myahudi kamwe hawezi kununua [wala kuuza] kitu chochote katika siku ya Sabato kuu. | √ | √ | X |
| 9 | Kadhalika, Nikodemo ananunua sanda katika siku ya kifo cha Kristo (Marko 15:46). Hata kama Yuda [Iskariote] ***labda*** alivunja Sabato, haiyumkini kabisa kwamba Nikodemo atanunua kitu chochote katika siku ya Sabato kuu (Nisan 15). | √ | √ | X |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10 | Maziko ya Yesu pia yalifanyika *katika* Siku ya Maandalizi na *kabla* ya Sabato (Luka 23:54; Yohana 19:42), na si *baada* ya machweo kama Nadharia ya Jumatano inavyoamini. Nadharia ya Ijumaa inajibu hoja hii kwa kudai kwamba siku hii ilikuwa ni Sabato ya wiki. Hata hivyo, Yoh. 19:31,42 inaweka wazi kwamba maziko yalifanyika [haraka] kabla ya machweo ili kuepuka kuvunja Sabato Kuu ya Nisan 15, na si Nisan 16. | X | √ | X |
| 11 | Katika Nadharia za Jumatano na Alhamisi, kila siku na matukio yake katika Wiki ya Mateso yanaelezeka bila mushkili, lakini katika Nadharia ya Ijumaa, siku ya Jumatano inakosekana kabisa! | √ | √ | X |
| 12 | Kristo alifufuliwa Jumapili (Marko 16:9), na si Jumamosi. | X | √ | √ |
| 13 | Siku hiyo ya ufufuo ilisemekana kuwa ni baada ya [zile] Sabato (plural / uwingi) kupita (Matt. 28:1) katika Kiyunani sisisi. Kuna Sabato moja tu katika Nadharia ya Ijumaa. | √ | √ | X |
| 14 | Kwa kuwa sikukuu ya Malimbuko ilikuwa ni karamu iliyofanyika hekaluni, yamkini ni kalenda ya *hekalu* ndiyo ilitumika na Wayahudi, badala ya ile kalenda ya baadaye sana ya Mafarisayo, katika kupanga sikukuu / karamu ya Malimbuko.[6] Masadukayo walitoa hoja sahihi pale waliposema kwamba Karamu ya Malimbuko daima ilipaswa kuangukia Jumapili (Walawi 23:9-14). Hoja nyingi zilizotolewa zimesimama katika kalenda ya Mafarisayo, ambayo imeiweka Karamu ya Malimbuko tarehe ya 16, bila kujali inaangukia siku gani ya wiki. | X | √ | X |
| 15 | Ufufuo wa Kristo na watakatifu wa Agano la Kale (tazama Matt. 27:53-54; Isaya 26:19; Hosea 6:1-3 pamoja na 1Wakor. 15:1-4; Yoh. 5:25; Waefe. 4:8-10; Waebr. 12:23) ulitajwa kutokea "takriban alfajiri" [7] (Hosea 6:3 [Kiebrania sisisi]; Marko 16:9; Yoh. 20:1 pamoja na Matt. 28:1; Luka 24:1. Aya hizi zinavuruga kabisa Nadharia ya Jumatano ambayo inalazimu Kristo kuinuka punde baada ya jua kuzama siku ya Jumamosi (!). | X | √ | √ |
| 16 | Kristo alisulibiwa mwaka 30 BK. Ingawa tarehe hii bado inajadiliwa, idadi kubwa zaidi ya wanazuoni wanaamini kwamba hii ndiyo tarehe inayokubaliana na ushahidi mkubwa wa Biblia. Ili kuona Ushahidi mkubwa wa kifo cha Bwana Yesu mwaka 30 BK, tafadhali soma kitabu changu, *December 25 Jewish Style.* | X | √ | √/X[8] |
| 17 | Jumapili ya Matawi haikuwa Sabato. Katika Nadharia ya Jumatano, kuingia Kwake Jerusalemu kwa shangwe kunaangukia Jumamosi. Hii haina uelekeo wa kuwa sahihi kwani inawahusisha wote, Kristo (Kumb. 5:14) na watu Wake (Hesabu 15:32-36) katika kuvunja Sabato. Kwa upande wa | X | √ | √ |

……………………………………………………………………..

[6] Karamu / Sikukuu ya Malimbuko ni kivuli (kiashiria kilichotangulia) cha ufufuo wa Yesu (1Wakor. 15:20,23). Kwa kuwa Karamu ya Malimbuko (siku aliyofufuliwa Kristo) ilikuwa ni Karamu ya hekalu[ni], basi kwa hakika kalenda ya hekalu ndiyo iliyotumika katika kupanga siku ya karamu hii, na si kalenda iliyotengenezwa na Mafarisayo baadaye sana. Kalenda ya hekali ilipanga Sikukuu ya Malimbuko daima iangukie siku ya Jumapili iliyoifuata tarehe ya Nisan 14. Katika mwaka 30 BK, siku hii iliangukia Jumapili, Nisan 17.

[7] Kutoka TWOT (Theological Wordbook of the Old Testament); neno la Kiebrania linalomaanisha "takriban".

[8] Watetezi wa nadharia mbalimbali za Ijumaa wanadai Kristo alisulibiwa wakati fulani kati ya 30 BK na 34 BK.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kristo itakuwa ni kushindwa kumpa mnyama Wake pumziko la Sabato na kwa upande wa watu itakuwa ni katika kukata matawi. | | | |
| 18 | Nadharia ya Ijumaa pia inashindwa kufanikisha Jumapili ya Matawi katika Nisan 10, na kunafanya kuingia Kwake Jerusalemu kwa shangwe kuangukie Jumatatu. | √ | √ | X |
| 19 | Kama Yesu hakufufuliwa Jumapili, basi hesabu ya siku hadi Pentekoste haiwezekani au tuseme inavurugika. | X | √ | √ |

**II. Muhtasari wa Wiki ya Mateso unaoonyesha kwamba Yesu aliendа kama ilivyopangwa.**

Siku kumi kabla ya kusulibiwa, Kristo alipakwa mafuta kwa ajili ya maziko Yake katika siku ile ile ambayo kondoo wa Pasaka walikuwa wakichaguliwa na kuwekwa wakfu kwa ajili ya kuchinjwa. Pia ni katika eneo lile lile.

Katika siku kumi zinazofuata, kondoo wale wanatazamwa na kuchunguzwa kila siku ili kuhakikisha kwamba hakuna dosari yoyote inajitokeza. Na kwa hakika kila siku katika siku kumi zinazofuata ina umuhimu, maana na utaratibu wake katika tafsiri [sahihi] ya Nadharia ya Alhamisi. Yesu alionekana / alitazamwa, na ingawa alishutumiwa kuwa ni mtenda dhambi, lakini hakupatikana na kosa lolote. Alichunguzwa na kuonekana hana dosari yoyote. Ila katika tafsiri ya Ijumaa kuna siku moja inakosekana, na watu wengine wanasema zinakosekana siku mbili.

Halafu kuna tukio la kuingia Yerusalemu kwa shangwe tarehe 10 Nisan. Kwa nini Yesu anatembea kuelekea kwenye hekalu? Kawaida, hii ndiyo siku ambamo kondoo walichungwa kuelekea hekaluni. Josephus (mwandishi Myahudi wa karne ya kwanza) anasema kwamba kulikuwa na kondoo zaidi ya 250,000 (laki mbili na hamsini) katika mitaa ya Yerusalemu wakiongozwa kuelekea hekaluni wakati Yesu akiwa anatembea katikati yao kuelekea huko huko hekaluni ambako makuhani walikuwa wakiwachunguza kondoo hao [kutafuta dosari]. Jambo la kustaajabu ni kwamba badala ya makuhani kuona dosari katika Yesu (Kondoo wa Pasaka), Yeye ndiye anaona dosari ndani yao na anasafisha hekalu kwa kuwaondoa humo. Yesu hatowaruhusu tena makuhani wale wafanye ibada pale hekaluni. Yeye ndiye Kondoo wa mwisho. Unapoweka picha kichwani ya Kondoo wa Mungu akitembea katikati ya wale kondoo 250,000, unaongezewa uelewa wa hisia kali iliyomo katika maneno ya Bwana Yesu pale anapozungumzia kifo Chake kinachokaribia, katika Yohana 12. Haya yote anayafanya katika ufahamu kamili wa nini maana na umuhimu wake. Alikuwa akitimiza unabii sambamba na ibada za karamu / sikukuu zilizoamriwa [hapo kale] kwa utimilifu halisi.

Na ukitazama chati ya Maana ya Pasaka, utaona kwamba kila kitu kilikuwa kinamlenga Yesu. Hii ni Chati # 1. Nitaisoma kwa haraka. Yeye alikuwa kondoo wa Mungu. Alikuwa kondoo asiye na doa. Alikuwa katika ujana Wake. Alipakwa mafuta siku 4 kabla ya Pasaka Yake. Alisulibiwa tarehe 14. Kama ambavyo Israeli wote walipaswa kumchinja mwanakondoo katika Kutoka 12:6, Israeli wote wanashitakiwa kwa kumwua katika Injli – kama ambavyo wewe na mimi tulimwua kwa dhambi zetu. Kama ambavyo damu ya kondoo ilipakwa katika nguzo za mlango, Maandiko yanasema kwamba damu ya Kristo ni lazima itumike katika Maisha yetu na kwamba inatulinda dhidi ya kuangamizwa na Mungu. Ni ukombozi *wa kaya*, kama ambavyo Kristo alizikomboa kaya nzima. Matendo 3:25 inasema kwamba Yesu atabariki familia zote za dunia, na hata Agano Jipya ni agano la familia. Kama ambavyo damu ilinyunyizwa / ilipakwa katika kizingiti cha mlango [wa kila kaya] na wale walioruka kizingiti hicho waliondoka Misri na kuyatoa maisha yao kwa Bwana na kwa ufalme Wake mpya, nasi tuinafanya hivyo leo, na kama tukikataa kufanya hivyo na kutaka kulitelekeza na kurudi ulimwenguni, Waebrania 10:29 inasema, "**Na Je, mnadhani ni adhabu kali kiasi gani anastahili kupewa mtu aliyemkanyaga Mwana wa Mungu chini ya nyayo zake, yeye aliyeifanya damu ya agano iliyomtakasa kuwa kitu najisi, na kumfedhehesha Roho wa neema**?" Tunaporuka kizingiti kile na kurejea nyuma [tulikotoka], tunaikanyaga damu Yake. Kama

ambavyo walipaswa kukaa ndani ya kaya ili wapate ulinzi katika Kutoka 12, tunapaswa [kuendelea] kukaa ndani ya kaya ya Kristo ili tuweze kupona / kuokolewa, kulingana na [kitabu cha] Waebrania. Kama ambavyo walipaswa kula nyama ya kondoo, nasi pia tunapaswa kula nyama ya Kristo. Kama ambavyo walipaswa kula nyama *yote*, Yoh. sura ya 6 inawaambia walalamikaji dhidi Yake kwamba tunapaswa kula nyama Yake yote. Hatuwezi kuchagua na kuchukua sehemu gani za Bwana tunazopenda. Hapana, tunapaswa kumchukua Yeye wote. Katika sura ile, Wayahudi wanaonekana walimtaka Yesu anayetoa riziki, na si [kama] Bwana, na si Mwokozi kutoka dhambi. Lakini Yesu aliwaambia ni lazima wawe washirika Wake kama Alivyo, na kama wanakwazika Naye, basi hawana wokovu. Kama ambavyo nyama ya kondoo ilichomwa kwa moto [kabla ya kuliwa], Kristo aliteseka katika moto wa hukumu ya Mungu. Kama ambavyo nyama ile ilipaswa kuliwa mara tu baada ya kutoka mekoni, Maandiko yanasema kwamba "leo" ndiyo siku ya wokovu na "sasa" ndiyo saa ya kumpokea Kristo. Kama ambavyo mboga chungu zililiwa kama kumbukumbu ya mateso yao katika utumwa Misri, Kristo anatukomboa kutoa katika uchungu wa dhambi. Yeye hakufa ili sisi tuwe na mazoea na dhambi; alikufa ili atuweke huru dhidi ya utumwa ule mchungu. Kama ambavyo makombo ya nyama ya kondoo yalipaswa kuteketezwa kwa moto ili yasiliwe na mgeni yeyote, sadaka ya Kristo inawagusa wateule pekee. Yesu alisema, "**Mimi nawaombea hao; siombi kwa ajili ya ulimwengu, bali wale ulionikabidhi, kwa kuwa hao ni wako**" (Yohana 17:9). Hakuna hata kipande kimoja cha yule Kondoo wa Pasaka kilichoruhusiwa kwenda kwa wale walio nje ya agano. Ufunuo 5:9 inasema tumegombolewa kutoka watu wa ulimwengo na kuwekwa mikononi mwa Mungu. Kama ambavyo [ilitakiwa kwamba] hata mfupa mmoja wa kondoo wa kafara usivunjike, Yohana 19 inasema kwamba huu ulikuwa ni unabii kwamba hata mfupa mmoja wa Kristo haukuvunjwa. Kama ambavyo Pasaka ilitakiwa kuliwa kwa haraka, [sisi] tunaonywa na Yesu kwamba tunapaswa kuwa tayari kuacha kila kitu na kumfuata Yeye. Kama ambavyo walikimbia kutoka Misri mara baada ya kula nyama ya kondoo, tunaitwa kuikimbia ghadhabu inayokuja. Kama ambavyo Misri ilihukumiwa na malaika wa kifo, wale wote ambao hawajagombolewa watahukumiwa. Kama ambavyo mlo wa Pasaka haukutiwa chachu, Kristo alipambana mara moja na chachu ya dhambi na kuweka chachu ya Ufalme Wake mahala pake. Na hii ndiyo sababu chachu iliwekwa katika mlo uluofuata – mlo / karamu ya Pentekoste. Kuenea kwa ufalme kunachukua nafasi ya kuenea kwa dhambi. Chachu ya ufalme siku ya Pentekoste inachukua nafasi ya chachu ya dhambi siku ya Pasaka. Hivyo walikula mkate usiotiwa chachu katika siku ya Pasaka, lakini walikula mkate uliotiwa chachu katika siku ya Pentekoste kama ishara ya mwanzo wa ufalme.

Nitarudia matukio fulani ili kuyajadili hivi punde, lakini kuna maana katika *wakati* ambao Kristo alipigiliwa misumari katika msalaba, pamoja na giza lililokuwako kutoka saa 6 hadi saa 9, yale masaa 3 ya giza.

Hayo [masaa 3] ndicho kipindi mahususi ambamo matayarisho yalikuwa yakifanyika ndani ya hekalu ili waweze kuchinja bila mushkeli zaidi ya kondoo 250,000 waliotakiwa kuchinjwa kati ya saa 6 mchana na saa 9 alasiri. Na uchinjaji ulipaswa kumalizika saa 11 ili wapate muda wa kutosha kurejea majumbani mwao, wasije wakavunja sabato ambayo huanza saa 12 jioni. Sasa, hao ni kondoo wengi sana ambao walipaswa kutayarishwa kati ya saa 6 mchana na saa 9 alasiri, na wachinjwe kati ya saa 9 alasiri na saa 11 jioni. Na Josephus anaripoti kwamba katika Pasaka yoyote palikuwa na takriban wasafiri [wa Kiyahudi] milioni 3 wanaotembelea Yerusalemu kutoka nchi mbalimbali za duniani.[9] Lakini si lazima watu wote hao wawepo katika hekalu. Kwa kuwa watu 10

………………………………

[9] Hivyo makuhani wakuu hawa, karamu yao ya Pasaka inapofika, ambapo wanachinja dhabihu zao kutoka saa 9 hadi saa 11 [yaani kutoka saa ambayo Yesu alikufa – kutoka saa 9 alasiri hadi saa 11 jioni. Hivyo walikuwa na masaa 2 - anaendelea], lakini ili kundi lisilopungua watu 10 watakula sadaka ya mnyama mmoja (kwani ni kinyume cha sheria kwa mtu mmoja kula peke yake), na wengi wetu hufikia watu 20 wanaofahamiana, (424) ikaonekana idadi ya dhabihu kuwa ni 256,400; (425) ambayo, ukipiga hesabu ya watu si zaidi ya 10 wanaokula nyama ya kondoo mmoja, inafikia

wanaweza kula kondoo mmoja, Josephus alisema kwamba kuwa na idadi ya watu 250,000 wanaopanga foleni wakingojea kupewa kondoo hekaluni ilikuwa ni kawaida sana wakati huu; mistari hii ya watu ilifika hata katika barabara zilizozunguka hekalu. Mungu alitaka kuhakikisha kwamba palikuwa na tamasha / shani ambayo taifa la Israeli lisingeweza kuikana.

Ili kuhakikisha makundi makubwa ya watu wanaokuwako wakati huu hawasababishi vurugu, makuhani walikuwa na mfumo wa mpangilio wa matukio yote, ulioanza saa 6 mchana. Na mfumo huu hautofanikiwa ikiwa hauanzi kutumika saa 6 kamili za mchana. Lakini nini kilitokea saa 6 kamili mchana? Giza nene; giza totoro. Taifa lilikumbwa na giza nene saa sita mchana (dakika ile ile ambayo kwa kawaida walikuwa wanaanza matayarisho yao, lilikuwa giza nene ambapo mwanga ulikosekana kabisa, na palikuwa na watu 250,000 wakisimama ndani na katika maeneo yaliyozunguka hekalu ambao hawakuweza kupiga hata hatua kwa kuogopa kukanyagana, na ambao hawakuwa na taa. Ni nani angefikiria kutembea na taa saa sita mchana!? Mungu anawapa masaa 3 kutafakari na kujiuliza ni nini kinaendelea katika Pasaka ya mwaka huu. Hakukuwa na namna yoyote ya kuondoka mahala pale. Na wala hawakutaka kuondoka kwa sababu walikuwa wanahitaji nyama ya kondoo [waliotakaswa]. Walikuwa ni watazamaji waliofungwa [na Mungu] ili washuhudie moja kati ya drama kuu kabisa za ulimwengu huu. Msomaji, je, unaanza kuuona msisimko ulioko katika kuelewa wendo (chronology) wa Mungu? Wendo ni funguo za kuelewa maandiko, na si vitu vya kuchosha akili.

Na pale walipopata ahueni mara Mungu aliporejesha mwanga mnamo saa 9 alasiri, yafuatayo ndiyo matukio waliyoshuhudia kwa macho na masikio yao (hapa naorodhesha matukio kwa kutumia vyanzo vyote kutoka karne ya kwanza – kama ambavyo uandishi mzuri wa Ernest Martin unavyoonyesha). Kutokana na vyanzo vya Jesephus, mwandishi wa historia wa Kirumi, pamoja na buku la Talmud, mashuhuda hawa takriban 250,000 wangeona milango ya nje ya hekalu ikifunguka yenyewe, wangesikia sauti kali ikisema, “Tuanaondoka mahala hapa,” (hii lazima iliwatisha sana, hili ni tukio la Wingu la Utukufu wa Bwana [Kut. 13:21-22; 40:34-35; 1Wafa. 8:1011] likiondoka), na hapo wangesikia vishindo vya tetemeko la ardhi, hapo wangeona lenta inayoshikilia pazia la nje yenye uzito wa tani kadhaa ikianguka chini (na pazia la nje likianguka pamoja nayo), na hapo ndipo wangeliona lile pazia la ndani likipasuka katikati, kutoka juu mpaka chini. Ilikuwa dhahiri ni Mungu ndiye aliyekuwa analipasua pazia lile kutoka juu mpaka chini. Huo ndio ulikuwa wakati wa kifo cha Kristo, na pia wakati huu ndio ulitakiwa kuwa wakati wa kuchinjwa kondoo [wale wote]. Lakini badala yake palikuwa na hofu, na hawakuweza kufanya kile walichopangiwa kufanya. Mungu hakutaka ushindani wowote dhidi ya Kondoo wake wa mwisho. (Matukio haya yote yanavurugika katika Nadharia ya Ijumaa).

Sasa, wakati huu pia ndio watu wale wangeiona sehemu ya ndani ya hekalu inayoitwa Mahala Patakatifu Zaidi. Wangeona ushoroba (corridor) yote. Bila kutegemea, macho yao yaliona sehemu ambayo hakuna mmoja wao aliota njozi ya kuiona. Maelfu ya makuhani walishuhudia tukio hili, na yaweza kuwa maelfu ya Wayahudi walipata fursa ya kuona ushoroba yote mpaka pale Mahala Patakatifu Zaidi. Jambo hili halikufanyika mafichoni. Na maana na umuhimu wake ulijulikana wazi na makuhani wale. Si jambo la kushangaza kwamba makuhani wengi sana walibadilika na kuwa Wakristo katika Matendo 6. Kwa kitendo hiki kimoja, Kristo alifuta mfumo wote wa dhabihu mbele za macho ya yeyote aliyeona.

………………………………
idadi ya watu 2,700,200 ambao walikuwa wasafi na waliotakaswa; (426) kwani kwa wale walio na ukoma (ugonjwa wa ngozi), ugonjwa wa zinaa / ngono wa gonorrhea, au wanawake walio katika vipindi vyao vya mwezi, au ambao kwa namna moja au nyingine wana uchafu unaowazuia kisheria kushiriki katika karamu ya dhabihu (427); hii ni pamoja na wageni wasio Wayahudi wanaokuja kuabudu. War (6.9.3).

Lakini pia kulikuwa na maandalizi ya Karamu ya Malimbuko (mavuno ya kwanza). Karamu ya Malimbuko ilikuwa siku ya Jumapili, lakini maandalizi yake yalikuwa ile jioni kabla Yesu hajasulibiwa (jioni ya Jumatano). Wazee walienda mashambani na kuiweka alama sehemu itakayovunwa kwa kufunga mazao yaliyosimama shambani kwa kamba. Na huo ndio usiku ambao Yesu alifungwa kamba na wazee wa Israeli. Ebu kisia ni wapi mazao yalikuwa yakifungwa. Nje ya Yerusalemu, upande wa juu wa kijito cha Kidroni. Sasa kisia ni mahala gani Yesu alifungwa kamba na wazee? Nje ya Yerusalemu, upande wa juu wa kijito cha Kidroni, katika bustani ya Gethsemane, ambayo ilikuwa na mpaka na shamba lile [la kale]. Hivyo masuke ya nafaka ya mazao yalifungwa jioni ile ambayo Yesu alifungwa.

Unaweza kuniambia malimbuko yalikatwa / yalivunwa lini na saa ngapi? Ilikuwa ni alasiri ya siku iliyofuata (yaani Alhamisi) kabla tu ya Sabato ya Pasaka kuanza, na ikiutangaza na kuukaribisha mwanzo wa Sabato ya Pasaka. Na wakati huo ndipo Kristo aliondolewa msalabani. Wakati ulikuwa unakaribia sana mwanzo wa Sabato na ndiyo maana walilazimika kumzika katika kaburi la jirani. Sasa nitanukuu sehemu ya wasifu wa mavuno ya Malimbuko iliyoandikwa na mwandishi wa Kiyahudi Alfred Edersheim:

> Wakati wa kukata masuke ulipowadia, … wakati jua linatua, wanaume watatu, kila mmoja akiwa na mundu na kikapu, walianza kazi. Katika kudhihirisha hali na tabia ya kipekee kabisa kuhusiana na ibada hii, kwanza waliwauliza watu waliosimama kando ya shamba (wapiti njia) mara tatu maswali haya: ‘Jua limetua?’ ‘Kwa mundu huu?’ ‘Katika kikapu hiki?’ ‘Katika Sabato hii (au siku ya kwanza ya Pasaka)?’ – na mwisho, ‘Nianze kuvuna?’ Baada ya kuitikiwa ‘ndiyo’ kwa kila swali, walikata ngano kiasi cha efah moja, au wastani wa kilo kumi na mbili (12kg).

Ukiufikiria uondoti huu wote, kwa mara nyingine tena unaona jinsi Mungu anavyosimamia hatma ya kila kitu kinachotokea. Ibada inayosimuliwa hapo juu ni kivuli cha tukio la wazee la ‘kumkata’ Kristo na kumwondoa kutoka kwa walio hai hapa duniani. Walikubaliana wafanye jambo hili katika kipindi cha Pasaka. Waliwauliza watu kama wautumie mundu (au la) na watu walikubali. Walichokubali katika mavuno ya ngano, walikikubali pia katika mauaji ya Yesu. Walipiga kele, “Msulibishe!” Watu wote waliutumia mundu ule kwa Yesu. Edersheim anazungumzia kinaya (irony) kinachoonekana hapa, kwamba kundi la watu walibeba kikapu cha ngano katika wakati ule ule ambao Nikodemo na Yosefu waliubeba mwili wa Kristo na kuupeleka mazikoni:

> “… kundi la watu waliopaaza sauti walitembea nyuma ya wajumbe kutoka Baraza Kuu [la Sanhedrin] nje ya mji na kuvuka kijito cha Kidroni. Wakati huo huo, kikundi kidogo cha waombolezaji kiliubeba mwili wa Mwokozi kutoka msalabani na kuupeleka katika kaburi lililochongwa mwambani ambamo hajazikwa mtu bado. Wakati kikundi kile kidogo kiliingia bustanini, huenda upande mmoja wa bustani hiyo, kundi lile kubwa, wakiendelea kupiga kelee, walitoka katika uwanda ulioko upande mwingine wa bustani unaovuka kijito cha Kidroni, ambao ulitengwa kwa lengo hilo. Hawa walitaka kujishughulisha na jukumu muhimu sana kwao. Yamkini kwa sababu ya mazingira haya Yosefu wa Arimathea alipouomba mwili wa Yesu, alikuwa na uhakika kwamba yeye, Nikodemo na wale wanawake hawataingiliwa katika jukumu lao la upendo wenye huzuni kubwa la kumzika Mwokozi wao.

Kikapu kizito killichojaa masuke ya ngano kilipelekwa hekaluni na ngano ile ilikaa hekaluni kwa siku tatu mchana na usiku, kama ambavyo Kristo alikuwa kaburini kwa siku tatu mchana na usiku. Kama ilivyokuwa ada, katika Jumapili ya kwanza baada ya Pasaka ngano ilitolewa kikapuni, ikapigwa, ikasagwa na kupepetwa. Halafu ikatolewa kwa Bwana kama sadaka ya kuinuliwa (wave offering). Ngano ni ishara ya muungano wa Yesu na watakatifu wote katika kifo, maziko, na ufufuo Wake. Na kama ambavyo ngano ile ilisagwa na kuwa kitu kimoja (unga) ambao hauwezi

kutenganishwa, sisi tumeunganishwa na Yesu katika namna ambayo hatuwezi kutenganishwa Naye. Kushiriki kwetu katika ufufuo Wake kunadhamini ufufuo wetu.

Uhakika wa sisi kupokelewa na Mungu kama sadaka ya kutikiswa ni sisi kuwa wamoja na Kristo kwa imani. Ni wale tu wanaoweka imani yao katika Kristo ambaye Maandiko yanasema juu yao kwamba mbele ya sheria walikufa, walizikwa pamoja na Kristo, na walifufuliwa pamoja na Kristo. Kutoka hapo na kundelea, hatma yetu sote inafungamana pamoja na Yesu. Waefeso inasema kwamba tunaketi pamoja na Kristo katika makazi ya mbinguni.

Je, hii si taswira adhimu ambayo Mungu ametupatia?

JEDWALI LA MAANA YA PASAKA

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Kondoo anachukuliwa (Kut. 12:3) | Kristo ni kondoo wa Mungu (Yoh. 1:29) |
| 2 | Asiye na dosari (Kut. 12:4,5) | Kristo hakutenda dhambi (1Pet. 1:19; 2Wakor. 5:21) |
| 3 | Mzaliwa wa kiume wa kwanza katika ujana wake (Kut. 12:5) | Kristo hakuwa mtoto – alikuwa mwenye nguvu & anayejitegemea – miaka ya thelathini |
| 4 | Alitengwa tarehe 10 Nisan – siku 4 kabla ya Pasaka (Kut. 12:3,4) | Kristo alipakwa mafuta siku 4 kabla ya Pasaka (kwa ajili ya maziko Yake) |
| 5 | Anachinjwa tarehe 14 Nisan (Kut, 12:6) | Alisulibiwa tarehe 14 (Yoh. 19:14,31) |
| 6 | Israeli yote walipaswa kumchinja kondoo (Kut. 12:6) | Israeli wote walimwua Kristo (Matt. 27:20-23; Luka 23:18; Matendo 2:23) |
| 7 | Damu ilipakwa kwenye nguzo za milango (Kut. 12:7,22) | Damu inapakwa kwenye mioyo (1Yoh. 1:7; Matt. 26:28; War. 5:9; Ufu. 1:5; 7:14) na ni ulinzi wetu (Ufu. 12:11) |
| 8 | Damu ilipakwa kizingitini (Kut. 12:7) na wale walioruka kizingiti waliondoka Misri na wakayaweka maisha yao mikononi mwa Bwana | Kamwe tusiikanyage damu ile yenye thamani (Waebr. 10:29) |
| 9 | Walipaswa kukaa ndani ili walindwe (Kut. 12:7) | Waebr. 3:6; 6:3-8; 10:36-39; etc |
| 10 | Walipaswa kushiriki katika mlo wa nyama ya kondoo (Kut. 12:8-10) | Hatuna uhai kama hatutoshirikiana na Kristo (Yoh. 6:53-55) |
| 11 | Waliamriwa kula nyama yote (Kut. 12:10) | Yohana 6 |
| 12 | Kondoo aliyebanikwa motoni (Kut. 12:8-9) | Kristo alihukumiwa msalabani (Waebr. 12:29; Isa. 53:5; 1Pet. 2:2) |
| 13 | Kuliwa mara baada ya kuiva – isiahirishwe mpaka asubuhi (Kut. 12:10) | Waebr. 3:7,12-15; 4:7 “Leo” 2Wakor. 6:2 “Sasa hivi” |
| 14 | Mboga chungu ili kukumbuka utumwa wao Misri (Kut. 12:8) | Kristo ametugomboa kutoka uchungu wa dhambi |
| 15 | Makombo yalipaswa kuteketezwa kwa moto. Kisibakie chochote kinachoweza kuliwa na mtu mwingine (Kut. 12:10) | Ukombozi ni kwa ajili ya wateule pekee. Ukombozi si wa wote (Ufu. 5:9-10; Yoh. 11:49-52; Yoh. 17:9-10) |
| 16 | Mungu alikataza kuvunja mfupa wowote wa kondoo (Kut. 12:46) | Yohana 19:32-33 |
| 17 | Mtakula mkiwa mmefunga mikanda kiunoni, mmevaa viatu vyenu, na mmeshika fimbo zenu (Kut. 12:11) | Tunapaswa kuwa tayari kuacha kila kitu na kumfuata Kristo |
| 18 | Iliwapasa kula haraka (Kut,. 12:11) | Matt. 3:7; nk. “Kimbieni ili mjiepushe na ghadhabu inayokuja” |
| 19 | Misri ilihukumiwa na malaika wa kifo (Kut. 12:12-13) | Wale wasiokombolewa watahukumiwa (Yoh. 3:18; nk) |


| | | |
|---|---|---|
| 20 | Mikate isitiwe chachu (hamira) – Kut. 12:8) | Kristo ametutakasa dhidi ya kuongezeka kwa dhambi (1Wakor. 5:5-7) |

**Hitimisho – Jinsi somo hili linavyoweza kutusaidia katika mwendo wetu wa Kikristo**

Somo hili linatusaidia kutambua usahihi na upatanifu wa Maandiko. Linatusaidia kutimiza 1Pet. 3:15, ambapo tunaamriwa tuwe tayari kutoa jibu la tumaini letu wakati wote. Linatusaidia kupambana na mashaka ya wenzetu. Linaimarisha imani yetu katika uweza na hekima ya Mungu. Lakini pia linatusaidia kuwa na matumaini katika neema za Mungu katika wakatu tunaoishi (sasa). Kama Mungu anaweza kusimamia na kufanikisha kwa utimilifu kabisa vipengele zaidi ya 100 vya tukio la kusulibiwa kwa Kristo, licha ya kwamba alikuwa akifanya kazi katikati ya matendo yenye dhambi ya wanadamu, bila ya Yeye mwenyewe kumshawishi mtu yeyote kutenda dhambi wala Yeye mwenyewe kujihusisha na dhambi, basi Anaweza kufanikisha jukumu la kutenda kila kitu kwa manufaa yetu leo hii. Tunaweza kumtumainia.

Kama ambavyo Yesu alikuwa na imani kamili kwa Mungu pale aliposema kwamba Yeye anaenda kama ilivyopangwa, nasi pia tunaweza kujiamini na kuwa na ujasiri unaotokana na kufahamu kwamba tunaenda kama ilivyopangwa. Hatuna haja ya kuogopa kuanguka kwa uchumi wetu [hapa Marekani] ingawa kuna uwezekano mkubwa wa jambo hili kutokea hivi punde (somo hili liliandikwa March 22, 2015). Hatuna haja ya kuuogopa ukomunisti. Hatuwezi kufa hata siku moja kabla ya ile siku ambayo Mungu amepanga, na hatuwezi kuteseka zaidi ya kiasi ambacho Mungu katika wema Wake ameruhusu. Ujumbe huu wote unapaswa kutuwezesha kutumainia katika neema na majaliwa ya Mungu kutoka mioyoni mwetu. Lakini kwa hakika tunapaswa kusimama katika heshima kuu, mshangao, na kusujudia hekima ya Mungu anayoidhihirisha katika Wiki ya Mateso. Kwa hakika tunapaswa kuitumia kila fursa tunayopewa katika kumtukuza kwa ajili ya msalaba wa Yesu Kristo.

Chati #1 na chati #2 ziko hapa chini:


CHRIST'S DEATH AT THE PASSOVER
As It Took Place In A.D. 30 -- A CHRONOLOGY
MONTH ABIB or NISAN
JEWISH CALENDAR DAYS
Each Day Begins At Sunset
(Days before Passover)
Regular Weekly Sabbath
ROMAN CALENDAR DAYS
Each Day Begins At Midnight
PASSOVER LAMB SELECTED
And Kept Until the 14th Day
CHRIST SELECTED
"TRIUMPHAL ENTRY"
Matt. 20:1-11
SUNDAY
MONDAY
TUESDAY
WEDNESDAY
(Customary
Pre-Passover Supper)
PASSOVER LAMB SACRIFICED
In The Afternoon of The 14th Day
"CHRIST
OUR PASSOVER
SACRIFICED FOR US"
I Cor. 5:7
THURSDAY
PASSOVER SUPPER EATEN
After Sunset Beginning The 15th Day
1st DAY —HIGH SABBATH
FRIDAY
(Reckoning of 3 Days
and 3 Nights)
Regular Weekly Sabbath
(Reckoning of Christ's
Resurrection The 3rd Day
After His Suffering)
SATURDAY
WAVE- SHEAF OFFERING
of The FIRSTFRUITS
On The Morning After The Sabbath
"CHRIST
THE FIRSTFRUITS
OF THE DEAD"
I Cor. 15:20, 23
SUNDAY
THE FEAST OF
UNLEAVENED BREAD
7 DAYS
BEGINNING OF THE
"COUNTING OF DAYS"
UNTIL PENTECOST
(50TH)
7th DAY —HIGH SABBATH
J.W.L. Jan. 1987

Note the Chart below
Which visually demonstrates the Relationship
Between the Wave Offering of Firstfruits and the Feast of Pentecost

Sunday, * Christ Risen, "Offering of the Omer," The "Counting of Days" begins.

| Sun. | Mon. | Tues. | Wed. | Thur. | Fri. | Sat. | (Sabbaths) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *1. | 2. | 3. | 4. | 5. | 6. | 7. | 1. |
| 8. | 9. | 10. | 11. | 12. | 13. | 14. | 2. |
| 15. | 16. | 17. | 18. | 19. | 20. | 21. | 3. |
| 22. | 23. | 24. | 25. | 26. | 27. | 28. | 4. |
| 29. | 30. | 31. | 32. | 33. | 34. | 35. | 5. |
| 36. | 37. | 38. | 39. | 40. | 41. | 42. | 6. |
| 43. | 44. | 45. | 46. | 47. | 48. | 49. | 7. |
| *50. | | | | | | 7 Sabbaths= 7 Weeks or 49 Days | |

Sunday, *50 a High Sabbath, "Pentecost" (50th), "Feast of Weeks" or "Feast of Firstfruits."

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Alhamisi mchana + Ijumaa usiku | = siku ya kwanza* |
| 2 | Ijumaa mchana + Jumamosi usiku | = siku ya pili |
| 3 | Jumamosi mchana + Jumapili usiku | = siku ya tatu |

Wayahudi walianza kuhesabu mwanzo wa siku kuwa ni baada ya machweo ya jua. Hivyo siku ilianza saa 12 jioni. Mchana + Usiku = siku moja.

Imetafsiriwa na Respicius Kilambo Luciani wa https://sayuni.co.tz
0679900814, 0754375474
Morogoro, Tanzania.

Kutoka somo la Biblia “He Must Suffer Many Things – Matthew 16:21” by Dr. Phillip G. Kayser of Dominion Covenant Church (DCC) of Omaha NE on March 22, 2015.

Ruksa ya kutafsiri kazi hii imetolewa na Dr. P. G. Kayser na inapatikana hapa:

© Copyright 2015 by Phillip G. Kayser. Permission is granted to individuals to download, print, or distribute this sermon on paper or electronically, provided that each reprint bears this copyright notice, current address, and telephone number, and provided that all such reproductions are distributed without charge. They may not be sold or issued in book form, CD-ROM form, or microfiche without prior permission. All rights reserved.
Phillip G. Kayser • Dominion Covenant Church • 307.N 41st Ave. Omaha, NE 68131 • 402.934.3300